


JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI  
WAKALA WA VYUO VYA MAFUNZO YA MIFUGO



---

---

**TAMBUA UGONJWA WA KUJARISHA  
DAMU (COCCIDIOSIS) UNAOATHIRI  
MIFUGO JAMII YA NDEGE**

---

---

Kimetayarishwa na:

Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA)  
Kampasi ya Morogoro  
S.L.P. 603,  
MOROGORO – TANZANIA  
E-mail: [litamorocamp@gmail.com](mailto:litamorocamp@gmail.com)

### **UTANGULIZI**

Ugonjwa wa kuharisha damu (coccidiosis) husababishwa na Protozoa aina ya Eimeria. Ugonjwa huu huathiri kuku wa kisasa na kienyeji.

Ugonjwa huu umekuwa ukirudisha maendeleo ya wafugaji wa kuku wa kisasa na wakienyeji kwa kusababisha vifo vingi Tanzania na duniani kote.

### **UGONJWA WA KUJARISHA DAMU NI NINI?**

- Ugonjwa huu wa kuharisha damu unawapata sana kuku.

### **UGONJWA HUU HUENEZWA VIPI?**

Ugonjwa huu huenea kutoka mnyama mmoja hadi mwingine kwa njia zifuatazo:

- Kula chakula chenye vimelea hai vya ugonjwa.
- Binadamu huweza kupeleka ugonjwa toka kwenye banda lenye ugonjwa hadi banda la kuku wasio wagonjwa kupitia viatu, mikono na nguo.
- Pia ugonjwa huweza kuenezwa na wadudu kama vile mende, panya, ndege na wadudu warukao.

### **JE, NI ZIPI DALILI ZA UGONJWA HUU?**

Dalili za ugonjwa huu zinaweza kuonekana waziwazi au kwa kujificha .

#### **Dalili hizo ni:**

- Kuku kuharisha kinyesi kilichochanganyika na damu na mara nyingine huharisha damu tupu.
- Kuku hudhoofika.
- Hatimaye huweza kufa.

### **ATHARI ZA UGONJWA**

- Kudhoofisha vifaranga na hata kuku wakubwa
- Vifo – kutokana na kupoteza damu nyingi.
- Kuku hupunguza utagaji wa mayai.

### **JINSI YA KUGUNDUA UGONJWA.**

- Fanya uchunguzi mara kwa mara kwa mifugo yako, mabadiliko yoyote ya kuku kinyesi.

- Peleka kuku wako wakafanyiwe uchunguzi kwenye maabara za mifugo ikiwa ni pamoja na kuku walio kufa ili wafanyiwe uchunguzi wa kina.

### **JINSI YA KUZUIA UGONJWA**

- Hakikisha mazingira ya mifugo kama vile mabanda na sakafu yanakuwa safi wakati wote.
- Kuku wagonjwa watengwe ili wasiwaambukize kuku wazima.
- Tumia dawa ya kinga.

### **JINSI YA KUTIBU UGONJWA WA KUJARISHA DAMU. (COCCIDIOSIS)**

- Kuku wagonjwa wanaweza kutibiwa kwa kutumia dawa kama vile Amprolium, Salfa na Esb3
- Dawa hizi zinaweza kuchanganywa kwene maji ya kunywa au chakula.

### **USHAURI**

Mfugaji unapokuwa na wasiwasi waone wataalamu wa mifugo kwa ushauri na huduma muhimu!